

Jua Linapotua

na

Hadithi Nyingine

(*Tafsiri*)

Mhariri: Miriam Osore



4

Vita vya Kukata Masikio

Miriam Osore

Moses Isegawa alizaliwa Uganda mnamo mwaka wa 1965. Sehemu kubwa ya maisha yake ya ujana aliishi Uholanzi (Netherlands) ambapo alikuza kipawa chake kama mwandishi na akatia fora katika uandishi wa fasihi. Lakini alitambua kwamba kiini cha msukumo wake kilikuwa jamii yake na kwa sababu hii, alirejea nyumbani kutangamana nao. Baadhi ya kazi zake zilizochapishwa ni riwaya za *Abyssinia Chronicles* na *Snakepit*.

6

Almasi

Miriam Osore

Anita Desai alizaliwa Mussoorie, sehemu ya milima iliyo Kaskazini mwa Delhi, mwaka wa 1937. Alianza kuandika katika Kiingereza akiwa na umri wa miaka saba. Hadithi yake ya mwanzo ilichapishwa akiwa na umri wa miaka tisa. Desai alisomea katika chuo kikuu cha Delhi ambapo alipata shahada yake ya BA katika fasihi ya Kiingereza. Riwaya yake ya kwanza, *The Peacock* ilichapishwa mwaka wa 1963, ikifuatiwa na *Voices of the City* (1965). Alipata tuzo ya *Guardian* kutokana na kitabu chake cha *The Village by the Sea* ambacho ni uandishi wa kubuni wa kazi za watoto. Katika mwaka wa 1978 alipata tuzo ya *National Academy of Letters* kutokana na uandishi wa *Fire on the Mountain*. Kwa sasa ni mwanachamá msomi wa *The Royal Society of Literature* kule London.

8

Mtaa wa Sandra

Miriam Osore

Michaeal Anthony, mwandishi mashuhuri na mwanahistoria, kutoka visiwa vya Caribbean, alizaliwa Mayaro, Trinidad na Tobago mnamo mwaka wa 1930. Mashairi yake ya kwanza yalichapishwa katika gazeti la *Trinidad Guardian* mnamo mwaka wa 1953. Mwandishi huyu alichapisha kitabu chake cha kwanza, *The Games were Coming* ambacho kilisifiwa sana na wahakiki na baadaye akachapisha riwaya, *The Year in San Fernando*. Anthony ameandika zaidi ya vitabu ishirini katika taaluma yake ya miongo minne. Hadithi hii ya *Mtaa wa Sandra* inapatikana katika mkusanyo wa hadithi fupi unaoitwa: *Cricket in the Road and Other Stories*.